# Alasiri Online

www.ippmedia.com

Jumatano Aprili 3, **2019**

Tanzani 500/- Kenya 50/-




# WOLPER

## AWAPOTEZA 'WAZUSHI'



# WOLPER AWAPOTEZA 'WAZUSHI'

Na Mary Kadoke

JACKLINE Wolper amefunguka issue ya kutovaa jezi uwanja wa taifa akiweka msimamo kuwa kazi yake ya ubunifu wa mavazi ndiyo iliyomsukuma kuvaa alivyovaa.

Amesema hayo alipofanya mazungumzo na Alairi Online baada ya kutupiwa lawama nyingi mitandaoni kuwa alitakiwa kuvaa jezi ya taifa katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kati ya Tanzania na Uganda yaliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Akifafanua zaidi kuhusu msimamo alioweka juu yamavazi yake amesema suala la kuvaa jezi si la lazima, muhimu la kuzingatia ni mtu kufika uwanjani na kuonyesha uzalendo kwa timu ya taifa.

"Nimeongea sana kuhusu hili, kuvaa jezi ni uzalendo? Kwani Watanzania hawajui nafanya kazi gani jamani mimi fundi cherehani na nilivaa vile kwa makusudi kabisa," amesema.

"Mimi kutokuvaa jezi haimaanishi sio mzalendo,"

ameongeza.

Kisa cha kurasa za umbea katika mtandao wa Instagram kumrushia kombora Wolper ni maamuzi yake ya kutovaa jezi tofauti na wasanii wengine wengi walioonekana kupigilia pamba hizo katika mechi hiyo.

Baadhi ya wasanii waliopongezwa kupendeza baada ya kuvaa pamba hizo ni Hamisa Mobetto, Jokate Mwegelo na Wema Sepetu.

Jack aliamua kuwa tofauti kwa kuvaa jinsi yake na blouse ya kitenge iliyoandaliwa na Wolper House of Stylish.

Pamoja na kuigiza, Wolper ni maarufu mjini kwa ubunifu wa mavazi, mpaka sasa ameweka rekodi ya kuvalisha mastar kibao kama Irene Uwoya, Nandy na Wema Sepetu.



# DIMPOZ ASAKA JIKO

Na Anaeli Mbise

Msanii wa kizazi kipya anayesumbua na ngoma mpya ya You are the best Ommy Dimpoz amesema kwa sasa yupo kwenye mchujo mkali wa kumpata mwanamke wa kuoa.

Akizungumza na Alasiri Online, Dimpoz amesema kwa sababu marafiki wake karibu wote wana familia anapambana kumpata mwanamke atakayemtunza kutokana na afya yake.

Amesema anahitaji mwanamke anayejua kupika uji, supu na hata kumjali mgonjwa kwa kila hali kwa sababu bado siyo mzima sana kiafya baada ya kuugua kwa muda mrefu.

"Unaweza kuangukia kwa mwanamke hajui hata kuandaa chakula cha mgonjwa itakuwa ni shida. Kwa sasa yaani nina chuja sana," amesema Dimpoz.

Kuhusu ukaribu wake na Msanii AY, kama atamshawishi na yeye kuoa nchini Rwanda, amesema atabaki nyumbani kwa kuwa bado kuna warembo wakali.

"Mimi sitakwenda nje mimi ni wenu tu haijalishi ni mkoa gani, lakini mimi nitaoa nyumbani," amesema Dimpoz.

# Master J akwepa kumsimama 'mamsapu'

Na Anaeli Mbise

PRODUCER wa muziki wa kizazi kipya Master J amefunguka kuwa hafikirii kusimamia kazi za mwanamuziki Shaa.

Akizungumza na Alasiri Online, Master J amesema kuwa kusimamia kazi za mwanamuziki huyo ambaye pia ni mke ni vingumu kwa sababu anahitaji uongozi ambao hatakuwa na mgongano wa masuala ya kifamilia.

"Unajua kumsimamia siyo issue ila yule ni mke wangu nahisi kama kuna vitu ambavyo havitakwenda sawa bora asimamiwe na meneja mwingine," amesema Master J.

Aidha producer huyo wa muda mrefu katika game ya Bongo fleva amesema kuwa ushauri wa namna ya kumfanya msanii huyo kutoa ngoma kali huwa anampa.

Mwanamuziki Shaa ametamba na ngoma kama vile Sugua Gaga, Siri ya Penzi pamoja na Subira.

# Harmonize ataka kutekwa



Na Anaeli Mbise

MWANAMUZIKI kutoka lebo ya WCB, Harmonize ameachia ngoma mpya inayojulikana kwa jina la Niteke.

Harmonize akizungumza na Alasiri Online, amesema kuwa video ya wimbo huo amecheza na mpenzi wake Sarah ili kudhihirisha jinsi anavyompenda kwa dhati.

"Hii ngoma ya sasa niko na mpenzi wangu tu tunacheza tukiwa beach and enjoying life bro mambo ni moto watu wanasema siku hizi nami nasema ni moto," amesema Harmonize.

Mwanamuziki huyo pia amesema ujumbe unaopatikana katika ngoma hiyo unazungumzia mwanamke alivyomteka kimapenzi.

Video ya ngoma hiyo imetengenezwa na Zoom production, ikiongozwa na director Kenny.



# TID

## APAKUA KITU CHA MOTO

**Na Anaeli Mbise**

MSANII wa muziki wa Bongo fleva Khalid Mohamed marufu kama TID pamoja na Q Chief wameachia video ya wimbo wa Najidai.

Akizungumza na Alasiri Online, TID amesema kuwa sababu kubwa za kuachia ngoma hiyo ni ujumbe ambao unaptikana unaomzungumzia mwanamke aliye kwenye mapenzi na mwanaume, hivyo kwa wapenzi hao kuwa ni furaha.

"Najidai maana yake halisi ni kuwa na amani moyoni ama nimepata ushindi kuwa na mpezni wangu tunaependana kwa dhati so I feel good," amesema TID.

Msanii Q Chief amesema kuwa ameshiriki katika chorus kutokana na kuipenda mistari ambayo iko katika ngoma hiyo.

"Unajua mimi na TID ni washikaji wa siku nyingi

nimefurahi kanipa shavu na ngoma yenyewe ni nzuri kama inavyojulikana ni kujidai tu," amesema Q Chief.

Ngoma hiyo imefanywa na producer T-touch na videoimefanyika katika fukwe za jiji la Dar es Salaam.

# ROMA AWAASA WASANII WAWABEBE MADOGO

**Na Mary Kadoke**

RAPA Roma Mkatoliki awasihi wanamuziki wenzake kuona thamani ya kusaidia chipukizi wanapohitaji msaada wao kwani wapo wasanii kibao waliofanikiwa kwa kupewa nafasi hapo awali.

Akifafanua hili alipofanya mazungumzo na Alasiri Online amesema huenda fursa hizo watakazotoa zikakuza muziki wao upande wa 'Collaboration'.

"Sioni ubaya wowote linapokuja suala la support kwa wasanii wachanga kwa sababu mwisho wa siku hainipunguzii chochote," amesema.

"Utamsaidia leo na kesho ukashangaa mkafanyacollaboration na ikafanya vizuri," amesema.

Akitoa mfano kuhusu mtazamo huo amesema miaka ya nyuma aliwahi kukutana na kijana aliyemfuata backstage na kumueleza jinsi gani alivyo na kiu ya kuimba na kukumbuka jinsi gani nguli Professor Jay alivyofungua

moyo wake kumsikiliza na kuchangia kumfikisha hapo alipo.

"Niliwahi kwenda sehemu nikakutana na dogo, alivyovaa na kuongea akanikumbusha miaka ya nyuma nilivyokutana na Professor Jay backstage na kuniachia namba zake ili nimtafute baadaye" amesema mkali huyu wa kibao cha Zimbabwe.

Akifanya mahojiano na chombo kimoja cha habari, Dogo Janja aliwahi kukiri kuwa Roma ana mchango mkubwa katika kukuza muziki wake na kumfikisha hapo alipo.





# BRIGHT

## ALIA KUCHOMA PESA

Na Mary Kadoke

MKALI wa ngoma ya Sina Bright amewaomba mashabiki kutoa full support ya kazi zake, kwani mara nyingi pamoja huwekeza pesa nyingi huangushwa na mapokeo ya kazi anazoachia.

Akifanya mazungumzo na Alasiri Online ameelekeza lawama zake kwa wasikilizaji na watazamaji wa kazi zake na kufuta kauli kuwa pesa ndio kikwazo cha kukuza muziki wake.

"Tunawekeza pesa nyingi kwenye muziki mafanikio madogo," amesema.

"Mafanikio kwenye muziki yanahitaji muda kwani pesa inayowekezwa ni kubwa, lakini kurudisha inachukua muda," amesema.

Akifafanua zaidi amesema mpaka sasa amefyatua kazi kibao, lakini mapokeo yake ni hafifu.

Orodha ya ngoma alizowahi kuachia ni Sina yenye watazamaji 273,356, katika mtandao wa YouTube, Ungaunga Mwana 298,000 na Subira 230,000.